



## Si halali damu ya muislamu isipokuwa kwa moja kati ya mambo matatu

Kutoka kwa bin Mas'udi radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake-: "Si halali damu ya muislamu isipokuwa kwa moja kati ya mambo matatu: Mzinifu aliyeo, na nafsi kwa nafsi, na mwenye kuacha dini yake mwenye kusambaratisha umoja".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Amebainisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa damu ya Muislamu ni haramu, isipokuwa akifanya moja katika mambo matatu: La kwanza: Akatakayetumbukia katika uchafu wa zinaa, na hali yakuwa ameo ndoa sahihi ya kisheria; ni halali kumuua kwa mpiga mawe. La pili: Atakayeua nafsi isiyo na hatia kwa makusudi pasina haki, atauwawa kwa sharti zake. La tatu: Mwenye kutoka katika umoja wa Waislamu; ima kwa kuacha dini yake ya Uislamu yote kwa kuritadi, au mwenye kutoka bila kuritadi kwa kuacha sehemu ya dini kama waasi, na vibaka, na wanaopiga vita Waislamu kama Makhawariji na wengineo.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/4714>

